*Jarida La*

# MIFUGO NA UVUVI

*#mifugonauvuviniutajiri*

TOLEO NO; WMU 0010| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

## Chanja zenye thamani ya milioni 117 zatolewa kwa wavuvi Kilwa





Mikataba ya uboreshaji kituo cha ukuzaji viumbe maji Kingolwira yasainiwa



Thamani mazao ya mifugo yapaa , Oman kinara

*Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu*

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni HALIUZWI

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi

# **Yaliyomo** Ndani **Jarida**


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri.............**Uk. 05 - 06** |
| 2 | Chanja zenye thamani ya milioni 117 zatolewa kwa wavuvi Kilwa .............**Uk. 05 - 06** |
| 3 | Mikataba ya uboreshaji kituo cha ukuzaji viumbe maji Kingolwira yasainiwa.......**Uk 07** |
| 4 | Utafiti wa wingi wa samaki Ziwa Tanganyika waanza rasmi..... **Uk. 08- 09** |
| 5 | SADC/WOAH waridhishwa na utekelezaji chanjo ya wanyama Tanzania ........... **Uk. 09** |
| 6 | Matukio katika picha ya makabidhiano ya chanja za kuanikia dagaa mkoani Lindi 26 Agosti, 2025........**Uk. 10** |
| 7 | Vibali vya uingizaji maziwa kutoka nje ya nchi vyapungua ...... **UK. 11** |
| 8 | Serikali yatumia teknolojia ya kisasa kudhibiti uvuvi haramu ........... **Uk. 12** |
| 9 | Elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi yafika Rorya.............. **Uk. 13** |
| 10 | Makusanyo sekta za mifugo na uvuvi yazidi kupaa .........**Uk. 14 - 15** |
| 11 | Wavuvi waanza kupewa elimu ulinzi rasilimali za uvuvi, Ziwa Victoria .......... **Uk. 16** |
| 12 | Rais Samia adhamiria kutatua changamoto ya ajira kwa vijana ....**Uk. 17-18** |
| 13 | Thamani ya mauzo sekta ya mifugo yapaa ........**Uk. 16** |
| 14 | Matukio mbalimbali katika picha...........**Uk. 17 - 20** |
















# Bodi ya Wahariri:

### Mwenyekiti
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### Mhariri
**Edward Kondela -** Afisa Habari Mwandamizi

### Msanifu
**Hamisi Hussein** - Afisa Habari

### Wajumbe
**Elibariki Mafole -** Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike -** Afisa Habari Mwandamizi
**Stanlay Bryaton -** Afisa Habari
**Chiku Makwai-** Afisa Habari



# Chanja zenye thamani ya milioni 117 zatolewa kwa wavuvi Kilwa

**Zina uwezo wa kukausha tani 3.7 za dagaa kwa siku**

**Na Omary Mtamike**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) imewawezesha wavuvi wa dagaa waliopo eneo la Kilwa Kivinje mkoani Lindi chanja 40 za kisasa za kuanikia dagaa zenye thamani ya shilingi milioni 117.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi chanja hizo iliyofanyika Agosti 21, 2025 wilayani Kilwa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema kuwa tukio hilo ni sehemu ya mkakati wa serikali unaolenga kuondokana na changamoto ya upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa na kuhakikisha dagaa zinazovuliwa kwenye eneo hilo zinakaushwa kwenye mazingira yanayozingatia usalama wa chakula.

"Natambua kuwa hapo awali dagaa mnaovua hapa walikuwa wakiharibika kutokana na kukaushiwa kwenye miundombinu isiyo rafiki na wakati mwingine walikuwa wakikutwa na mchanga au matope jambo ambalo mbali na kupunguza thamani ya mazao hayo sokoni lilikuwa likihatarisha afya za walaji hivyo hatua hii itamaliza changamoto hizo zote." alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

Aidha Mhe. Dkt. Kijaji aliwataka wanufaika wa miundombinu hiyo kuhakikisha wanaitunza na kuitumia kama ilivyokusudiwa ili iweze kuwanufaisha kwa muda mrefu zaidi na kukidhi malengo ya kutolewa kwake.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainab Telack aliishukuru serikali na Shirika la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kwa kuwawezesha wavuvi wa mkoa wake miundombinu hiyo ambapo mbali na kuahidi kusimamia matumizi yake aliwataka wavuvi hao kuhakikisha wanakuza uchumi wao kupitia chanja hizo.

"Ndoo moja ya dagaa wabichi sasa inauzwa kati ya shilingi elfu 40 hadi elfu 45 na wavuvi wetu wanauza kwenye nchi za Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Burundi hivyo hatukuwa na

Endelea Ukurasa. 06 >>>

>>> Kutoka UK. 05

# Chanja zenye thamani ya milioni 117 zatolewa kwa wavuvi Kilwa

tatizo la soko bali ilikuwa namna ya kuongeza thamani ya mazao yetu jambo ambalo leo limeanza kushughulikiwa kupitia ugawaji wa chanja hizi." aliongeza Mhe. Telack.

Mbali na chanja hizo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuboresha mazingira ya shughuli za uvuvi nchini ikiwa ni pamoja na kujenga masoko na maghala ya kuhifadhia samaki, vyumba vya kuhifadhi ubaridi, mitambo ya kuzalisha samaki na teknolojia za ukaushaji wa mazao ya uvuvi.





Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (kushoto) akifungua turubai linalotumika kulinda ubora wa dagaa wakati wa mvua muda mfupi kabla ya kukabidhi chanja za kisasa za kuanikia dagaa kwa wavuvi wa Kilwa mkoani Lindi Agosti 21, 2025. Kulia anayeshuhudia ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Zainab Telack.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena (kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya EF. IMER CONSTRUCTION CO. LTD, Bw. Emmanuel Pallangyo wakisaini mkataba wa uchimbaji wa visima vya maji katika kituo cha ukuzaji viumbe maji Kingolwira mkoani Morogoro, hafla iliyofanyika ofisi za wizara zilizopo Mtumba jijini Dodoma Agosti 29, 2025.

# MIKATABA YA UBORESHAJI KITUO CHA UKUZAJI VIUMBE MAJI KINGOLWIRA YASAINIWA

**Na, Hamisi Hussein**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Agnes Meena amewataka makandarasi watakaotekeleza miradi ya ukarabati wa vitotoleshi vya vifaranga vya samaki, ujenzi wa mifumo ya hewa kwenye mabwawa ya kufugia samaki, uchimbaji wa visima vya maji eneo la Kingolwira mkoani Morogoro na ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi katika Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na kuzingatia ubora.

Bi. Meena alisema hayo Agosti 29, 2025 katika ofisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma, mara baada ya kusaini mikataba minne na makandarasi hao ambapo aliwasisitiza kuzingatia muda na ubora wa miradi kulingana na makubaliano ya mkataba.

“Miradi hii ya kimkakati kwa wizara yetu na kama mnavyojua inawagusa moja kwa moja wananchi hivyo mtekeleze kwa kuzingatia muda na ubora wa mikataba ili iwanufaishe wananchi wetu.” alisema, Bi. Meena.

Kwa upande wao makandarasi wa miradi hiyo wameahidi kutekeleza mikataba yao kwa wakati na kuzingatia ubora ili ianze kufanya kazi kwa muda uliokusudiwa.

Mikataba iliyosainiwa ni pamoja na mkataba wa kuchimba visima viwili vya maji eneo la Kingolwira Mkoani Morogoro unaotekelezwa na Kampuni ya EF. IMER CONSTRUCTION CO. LTD, mkataba wa ujezi wa mifumo ya hewa katika mabwawa ya kufugia samaki Kingolwira unaotekelezwa na kampuni ya Kanuta Engineering and Supply Limited.

Mikataba mingine ni ile ya ujenzi wa vitotoleshi vya vifaranga vya samaki Kingolwira mkoani Morogoro, unaotekelezwa na Kampuni ya KPM investment LTD na ujenzi wa soko la samaki eneo la Kipumbwi katika Wilaya ya Pangani mkoani Tanga ambao unatekelezwa na Kampuni ya WCEC LIMITED

> ***“Miradi hii ya kimkakati kwa wizara yetu na kama mnavyojua inawagusa moja kwa moja wananchi hivyo mtekeleze kwa kuzingatia muda na ubora wa mikataba ili iwanufaishe wananchi wetu.”***
>
> Bi, Agnes Meena - Katibu Mkuu

# UTAFITI WA WINGI WA SAMAKI ZIWA TANGANYIKA WAANZA RASMI








Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede, akihutubia wadau wa Sekta ya Uvuvi, wakati wa hafla ya uzinduzi wa utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika, Agosti 27, 2025, mkoani Kigoma.

**Na, Stanley Brayton**

Nchi zilizopo ukanda wa Ziwa Tanganyika ambazo ni Tanzania, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Burundi, zimezindua rasmi zoezi la utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika, ambapo zoezi hilo linalenga kutambua wingi wa mazao ya uvuvi katika ziwa hilo.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki Ziwa Tanganyika, Agosti 27, 2025 mkoani Kigoma, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede alisema serikali imeelekeza kufanya tathmini ya wingi wa samaki waliopo Ziwa Tanganyika ili kujua wametawanyikaje na kwenye maeneo yapi, pamoja na kujua takwimu sahihi za wingi wa samaki katika ziwa hilo.

“Utafiti huu utahusisha mazao ya uvuvi aina ya migebuka, dagaa au samaki wanaoelea wa tabaka la juu, ili kusaidia uwekezaji wenye tija kwa takwimu na kuvutia wawekezaji.” alisema Dkt. Mhede.

Aidha, Dkt. Mhede aliweka bayana kuwa zoezi hilo halifanywi tu kwa ajili ya kuandika ripoti, bali kupata ushahidi wa kusaidia katika uundaji wa sera, ikiwemo kujua namna ya kuendeleza Ziwa Tanganyika, kuhifadhi ziwa na rasilimali zake au matumizi ya rasilimali hizo.

Vilevile, Dkt. Mhede alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imejipanga kikamilifu kwa kuandaa wataalamu wa kutosha ili kuhakikisha utafuti huo unakamilika kwa mafanikio.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Mohamed Sheikh alisema, katika miaka ya 90, Tanzania ilifanya utafiti kama huo, na kubaini kuwa wingi wa samaki ulikuwa tani 303,645, na kwamba ongezeko la watu, mabadiliko ya tabia nchi na ongezeko la nguvu ya uvuvi huenda ndio vimefanya mazao hayo kupungua kutokana na uhitaji kuongezeka zaidi.

Prof. Sheikh alisema tangu wakati huo hakuna tathmini kama hiyo ya kikanda

iliyofanyika kutokana na uhaba wa rasilimali, ambapo Mwaka 1995 Tanzania ilikadiriwa kuwa na tani 157,493 na idadi hiyo ilipungua hadi tani 144, 690 kwa Mwaka 2022 na baadae ilipungua zaidi hadi tani 84,094 katika utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

Halikadhalika, Prof. Sheikh, alisema suala la kufanya utafiti wa wingi wa samaki katika Ziwa Tanganyika utasaidia kujua idadi ya samaki waliopo katika ziwa hilo, ili kuweka mipango madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kuhakikisha uendelevu.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa TAFIRI Dkt. Ismael Kimirei alisema mafunzo ya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika yalifanyika kwa siku kumi, ikijumuisha kuweka sawa mitambo ya kufanyia utafiti na kuandaa mpango kazi wa utafiti huo.

Dkt. Kimirei alisema utafiti huu ni muhimu kwani unasaidia katika kuhuisha takwimu za wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika na kuwezesha serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wanachama wa nchi za Ziwa Tanganyika kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika ziwa hilo.



# SADC/WOAH waridhishwa na utekelezaji chanjo ya wanyama Tanzania




Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini Dkt. Benezeth Lutege akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya chanjo na utambuzi wa mifugo kitaifa, wakati wa mkutano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Agosti 26,2025 Lusaka nchini Zambia.

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Shirika la Kimataifa la Afya ya Wanyama (WOAH) zimeridhishwa na utekelezaji wa kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo inayotekelezwa nchini.

Hayo yalifahamika mara baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya utekelezaji wa kampeni hiyo na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini Dkt. Benezeth Lutege wakati wa mkutano wa nchi hizo ulioandaliwa na WOAH kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Afrika linalojishughulisha na Sekta ya Mifugo na Uvuvi (AU-IBAR) uliofanyika jijini Lusaka nchini Zambia Agosti 26, 2025.

Hatua hiyo imeipandisha Tanzania kutoka hatua ya pili hadi ya tatu kuelekea kutokomeza ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo ifikapo mwaka 2030.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Makabidhiano ya chanja za kuanikia dagaa yalifonywa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe . Dkt. Ashatu Kijaji mkoani Lindi 26 Agosti, 2025











# Vibali vya uingizaji maziwa kutoka nje ya nchi vyapungua



**Na. Elibariki Mafole**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Bodi ya Maziwa (TDB) imeendelea kusimamia biashara ya maziwa nchini ambapo jumla ya lita za maziwa 90,416,788.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 226 zilisindikwa na kuuzwa katika masoko ya ndani ya nchi.

Aidha, vibali vya kuingiza maziwa kutoka nje ya nchi vimepungua kutoka 782 vyenye jumla ya lita 11,747,150 zenye thamani ya shilingi 23,423,652,811.8 Mwaka 2023/2024 hadi vibali 630 vyenye jumla ya lita 10,089,767.50 zenye thamani ya shilingi 22,969,085,568.85.

Kupungua kwa kiasi cha maziwa yanayoingizwa nchini kutoka nje ya nchi kunatokana na juhudi za serikali za kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi, hivyo kuwezesha ongezeko la usindikaji ndani ya nchi.

Kwa sasa, kiwanda cha kusindika maziwa cha ASAS Dairies kimeanza uzalishaji wa maziwa ya unga ambapo kina uwezo wa kusindika lita 100,000 za maziwa ya unga kwa siku.

Kuimarika kwa biashara ya mazao ya mifugo nchini kwa mwaka 2024/2025, kulichangia kuongezeka kwa ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka, mathalani kiwango cha unywaji wa maziwa kiliongezeka kutoka wastani wa lita 67.5 Mwaka 2023/2024 hadi lita 68.1 Mwaka 2024/2025,

Pamoja na ongezeko hilo, ulaji wa mazao hayo bado haujafikia viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ambavyo ni lita 200 za maziwa kwa mtu kwa mwaka.

# Serikali yatumia teknolojia ya kisasa kudhibiti uvuvi haramu

**Na, Edward Kondela**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ikiwa kwenye jitihada za kuimarisha usimamizi, uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi yakiwemo mazalia na makulia ya samaki, katika Mwaka 2024/2025, ilitumia kiasi cha shilingi milioni 259,600,000 kwa ajili ya kutumia teknolojia ya kisasa kudhibiti uvuvi haramu kwa kununua ndege nyuki (drone), kutoa mafunzo kwa waendeshaji, kufunga vituo vya kudhibiti, kufanya usajili na kuanzisha mfumo wa kuhifadhi na kuchambua taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ndege hiyo.

Ndege nyuki hiyo iliyosajiliwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA) kwa namba 5H-25038 ambayo imeunganishwa na mfumo wa ufuatiliaji wa wavuvi, ina uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 400 na kukaa angani kwa muda wa saa mbili na kuchukua picha mnato na mjongeo za kiwango cha juu za vyombo vya uvuvi, uhalifu wa uvuvi na utoroshaji wa mazao ya uvuvi.

Pia, itaongeza ufanisi katika kusimamia rasilimali za uvuvi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za doria na muda wa kukusanya taarifa na matukio katika maeneo ya uvuvi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ndege nyuki hiyo jijini Mwanza Aprili 13, 2025 kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa wizara hiyo Mhe. Alexander Mnyeti alisema serikali iliamua kuchukua hatua madhubuti za kisasa kuhakikisha inadhibiti uvuvi haramu kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Aidha, alisema mpango wa matumizi ya ndege nyuki hautaishia Ziwa Victoria pekee, bali kupeleka matumizi hayo katika Ziwa Tanganyika na Nyasa, pamoja na maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi ili kuhakikisha kila pembe ya nchi inaonja matunda ya teknolojia ya kisasa katika usimamizi wa rasilimali.

Pia, alisema ndege nyuki hiyo ina uwezo wa kutoa taarifa kulingana na muda halisia na kwamba itasaidia kupunguza vitendo vya uvuvi haramu na gharama za uendeshaji wa doria ziwani pamoja na kutumika katika masuala ya utafutaji na uokoaji.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede akizungumza katika hafla hiyo alisema uwepo wa ndege nyuki unaenda sambamba na takwa la kidunia la matumizi ya teknolojia rafiki za kimazingira.

Alifafanua kuwa katika mapambano ya uvuvi haramu serikali ililazimika kutumia boti na magari yanayotumia mafuta ya diesel ambayo yanaleta hewa ya ukaa kwa kiasi kikubwa ila kwa matumizi ya ndege nyuki, itakuwa ikienda eneo mahsusi ambalo kuna viashiria vya uvuvi haramu hivyo kupunguza matumizi ya boti na magari kwa ajili ya kuwasaka wavuvi haramu.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), iliimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za uvuvi ili kupanga mipango madhubuti na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi ambapo ilitoa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu za uvuvi katika maeneo ya Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Bwawa la Mtera, Ziwa Manyara, Mto Mara pamoja na kufanya sensa za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Bwawa la Mtera, Ziwa Manyara, Mto Mara, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa na maji madogo (Bwawa la Nyumba ya Mungu, Ziwa Babati, Ziwa Eyasi, Ziwa Natron na Ziwa Tlawi).

Halikadhalika, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA), imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu, kwa kutumia mifumo ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli na kuweka waangalizi wa uvuvi kwenye meli zilizopewa leseni, pamoja na kufanya ukaguzi wa meli za uvuvi zilizoomba leseni na vibali katika bandari za Dar es Salaam, Zanzibar na Victoria - Ushelisheli.

Pia, wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kuboresha usimamizi wa rasilimali za bahari kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika kufanya doria.

Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, MPRU imeanzisha kanzidata kwa ajili ya usimamizi wa matumbawe nchini pamoja na kuandaa mpango wa kitaifa wa miaka mitano kwa ajili ya uhifadhi wa rasilimali za bahari na kuanzisha kituo cha kitaifa kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za bahari hususan matumbawe.

Haya yote yanafanyika katika kusimamia uvuvi wa Bahari Kuu, unaofuata taratibu na sheria za nchi na kudhibiti viashiria vya uvuvi haramu na matumizi ya vifaa visivyotakiwa kisheria pamoja na meli kutovua maeneo ya mazalia ya samaki.

Mafanikio yanayopatikana katika kulinda na kusimamia rasilimali za uvuvi, yanatokana na ushirikishwaji thabiti wa wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi wakiwemo viongozi wa ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa,





Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU's) na Asasi zisizo za kiserikali (NGO).

Katika kudhibiti matukio ya uvuvi haramu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kukamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Uvuvi, sura 279, yakijumuisha kipengele cha kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji Tanzania ambayo itakuwa na jukumu la kuendeleza, kusimamia, kudhibiti, na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepewa jukumu la kuimarisha uhifadhi, ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bahari ya Hindi, mabwawa ya Nyumba ya Mungu pamoja na Mtera.

Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali, imekuwa ikifanya doria katika maeneo hayo kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo za majini, nchi kavu na angani ili kudhibiti uvuvi haramu unaohusisha samaki ambao hawakidhi vigezo vya kuwa sokoni, vifaa visivyothibitishwa kwa ajili ya uvuvi pamoja udhibiti wa kuvua maeneo ya mazalia ya samaki na viumbe maji vingine.

Kwa upande wa ukanda wa Bahari ya Hindi, wizara ilivunja rekodi ambapo katika mwaka huo wa fedha ilifanikiwa kuondoa uvuvi haramu wa kutumia vilipuzi ambapo kwa sasa hali hiyo imedhibitiwa kuanzia vyanzo, wasambazaji na watumiaji wa vilipuzi na kwa zaidi ya mwaka mmoja hakuna matukio ya uvuvi huo kwa ukanda wote wa Bahari ya Hindi, pamoja na kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji ili uhalifu huo usiendelee siku zijazo.

Katika maziwa makuu, wizara inaendelea na kazi ya kusafisha na kuondoa zana haramu za uvuvi, ambapo kazi hiyo imefanikisha kugundua na kunasa mtandao mpana wa uingizaji wa nyavu haramu ambazo hutumika kwa uvuvi haramu.

Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kuimarisha usimamizi wa maeneo ya mazalia na makulia ya samaki katika Ziwa Victoria kwa kuweka alama zinazobainisha mipaka ili kudhibiti shughuli za uvuvi na uharibifu wa mazingira.

Hatua hiyo itawezesha samaki kukua na kuzaliana ambapo katika mwaka 2024/2025 kwa kuanzia, wizara ilinunua na kusanikisha jumla ya maboya 32 ambayo yaliwekwa kwenye maeneo ya mazalia ya samaki katika Halmashauri za Misungwi na Nyamagana, mkoani Mwanza.

Wizara, inaendelea kuwashukuru na kuwakumbusha wadau wa sekta ya uvuvi kuzingatia sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za taifa na kwamba itaendelea kusimamia sekta hiyo na kuunga mkono juhudi za wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi.

# Elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi yafika Rorya

## Na, Hamisi Hussein

Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bw. Kimasa Bugomba amesema ulinzi wa rasilimali za sekta ya uvuvi utasaidia kuongeza upatikanaji wa mazao ya uvuvi na kuchochea uchumi wa wananchi na pato la taifa.

Akitoa elimu ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa ukanda wa Ziwa Victoria Agosti 26, 2025, kwa wavuvi na wachakataji wa mazao ya uvuvi katika Mwalo wa Isegere uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Bw. Bugomba alisema wajibu wa kulinda rasilimali za uvuvi ni jambo shirikishi baina ya wadau na serikali kutokana na umuhimu wake kiuchumi.

"Wizara yetu kwa Mwaka 2025/2026 katika vipaumbele tulivyonavyo ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi kwa kutumia teknolojia, ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kwa hiyo sisi serikali na nyie wadau wa uvuvi tunawajibika kulinda rasilimali hizo ili sote tunufaike kiuchumi" alisema Bw. Bugomba.

Awali, akiwa ofisini kwake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Dkt. Khalfanis Ilekizemba aliiambia timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa sekta ya uvuvi inachangia shilingi bilioni 1.8 kwenye mapato ya halmashauri hiyo na kuahidi kuiunga mkono wizara juu ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

"Tunashukuru wizara kuendelea kuelimisha juu ya ulaji wa samaki kwa jamii zetu na sisi tutatoa ushirikiano kuanzia kwenye ulinzi wa rasilimali za uvuvi na kuhimiza watu wetu wale samaki." alisema Dkt. Ilekizemba.



Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bw. Kimasa Bugomba akitoa elimu ya athari za uvuvi haramu kwa wavuvi wa Isegere Rorya, Mkoani Mara Agosti 26, 2025.

Akiwa kwenye mwalo huo wa Isegere, Mfawidhi wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Kituo cha Mkoa wa Mara Bw. Yohana Mirumbe, aliwambia wavuvi, wamiliki wa vyombo vya uvuvi na wadau wote wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi kuzingatia sheria na taratibu za ukataji wa leseni na matumizi sahihi ya zana za uvuvi ili kuondokana na uvuvi haramu.

Alisema kuna baadhi ya wavuvi hutumia nyavu zinazoruhusiwa kisheria lakini wanazitumia kuvua maeneo yasiyoruhusiwa akitolea mfano kutumia wavu wa kuvulia dagaa kwenda kuvulia samaki aina ya sangara akisisitiza kuwa ni kosa kisheria.

Kwa upande wake Afisa Uvuvi Mkuu ambaye anasimamia udhibiti ubora na masoko (QC) mkoani Mara Bw. Mkinze Rajabu alielezea vigezo vya ubora wa mazao ya uvuvi yanayokidhi ushindani wa soko ambapo aliwaelimisha wadau wa uvuvi njia za kudhibiti ubora na jinsi ya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

Baadhi ya wavuvi na wachakataji wa mazao ya uvuvi katika mwalo huo waliipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kutoa elimu hiyo pamoja na kusikiliza changamoto zinazowakabili na kuiomba serikali kuongeza jitihada za ufutiliaji na usimamizi wa sheria za uvuvi ili kutokomeza uvuvi haramu katika ukanda wa Ziwa Victoria.

# MAKUSANYO SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI YAZIDI KUPAA

Na, Edward Kondela

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiwa ni moja ya wizara muhimu katika sekta za uzalishaji, imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwa pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, katika vipindi vyote vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan katika awamu ya sita inayoongozwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Moja ya mambo muhimu ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikitekeleza ni kuhakikisha inafikia malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuiwezesha serikali kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kutokana na hilo, uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi umekuwa ukihakikisha unafikia malengo ya serikali kwa usimamizi imara wa ukusanyaji wa maduhuli pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ili kuchangia katika pato la taifa.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliweka rekodi ya makusanyo ya maduhuli ya shilingi 68,328,435,362.07 sawa na asilimia 99 ya lengo la kukusanya shilingi 69,105,000,000.

Tukiangazia sekta ya mifugo kuanzia Julai 1, 2024 hadi Juni 30, 2025, ilikusanya shilingi 35,658,450,089.79 sawa na asilimia 98.76 ya lengo la kukusanya shilingi 36,105,000,000.00 katika sekta hiyo.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikisimamia maduhuli kwenye minada iliyopo chini yake ikiwemo ya upili, mpakani na awali.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, kwenye minada ya upili ya Pugu (Dar es Salaam), Kizota (Dodoma), Ipuli (Tabora), Igunga (Tabora), Nyamatala (Mwanza), Mhunze (Shinyanga), Themi (Arusha), Meserani (Arusha), Weruweru (Kilimanjaro), Buzirayombo (Geita), Nata (Tabora), Sekenke (Singida), Lumecha (Ruvuma) na Rukole (Kagera), Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikusanya shilingi 3,400,275,500.00 sawa na asilimia 93.10 ya lengo kwa mwaka.

Aidha, katika minada ya mpakani ya Kirumi (Mara), Kasesya (Rukwa), Longido (Arusha), Mutukula (Kagera), Waso (Arusha), Horohoro (Tanga), Magena (Mara), Murusagamba (Kagera) na Kileo (Kilimanjaro) ilikusanya Shilingi 300,156,300.00 sawa na asilimia 87.38 ya lengo kwa mwaka.




Hali kadhalika, kwenye minada ya awali Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilikusanya shilingi 16,800,625,064.91 sawa na asilimia 88.42 ya lengo walilowekewa kwa mwaka huo.

Idara ya Huduma za Mifugo kupitia ofisi zake za kanda zilizopo mikoa ya Arusha, Iringa, Mtwara, Mwanza, Sumbawanga (Rukwa), Tabora, Temeke (Dar es Salaam), Dodoma, pamoja na Dodoma makao makuu katika mwaka huo wa fedha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilifanikiwa kukusanya shilingi 12,871,534,907.38 sawa na asilimia 101.22 ya lengo.

Vituo vya ukaguzi na bandari, Kyaka (Kagera), Lamadi (Simiyu), Kibaha (Pwani), Marendego (Lindi), Makuyuni (Arusha), Ndelema (Tanga), Bagamoyo (Pwani), Mnazi Mmoja, Ruvu (Dar es Salaam), Rusumo (Kagera), Kibirizi (Kigoma), Sirari (Mara) pamoja na bandari za Dar es Salaam, Tanga, Kirando (Rukwa) na Kigoma, wizara ilikusanya shilingi 283,978,850.00 sawa na asilimia 91.14 ya lengo kwa mwaka.

Pia, serikali kupitia mashamba inayomiliki ya Nangaramo (Mtwara), Mabuki (Mwanza), Kitulo (Mbeya), Ngerengere (Morogoro), Sao Hill (Iringa), Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) Arusha, Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya), ambayo yamekuwa yakizalisha mifugo, mbegu za mifugo pamoja na malisho yaliweza kukusanya shilingi 1,932,456,467.50 sawa na asilimia 128.83 ya lengo kwa mwaka.

Zao la ngozi nalo halikuwa nyuma katika ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo zilikusanywa shilingi 69,423,000.00 sawa na asilimia 85.83.

Kwa upande wa sekta ya uvuvi katika mwaka wa fedha 2024/2025, kuanzia Julai 1, 2024 hadi Juni 30, 2025 Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikusanya shilingi 32,669,985,272.28 sawa na asilimia 99.00 ya bajeti lengwa ya shilingi 33,000,000,000.00.

Tangu serikali ya awamu ya sita iingie madarakani chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akifanya ziara nchi mbalimbali na kuhamasisha kufunguliwa kwa milango ya kibiashara kwa bidhaa za Tanzania kuuzwa nje ya nchi.

Kufuatia hali hiyo katika mwaka wa fedha 2024/2025 leseni za uvuvi na uuzaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi, zilikusanywa shilingi 934,088,932.27 sawa na asilimia 45.37 ya lengo kwa mwaka, kutokana na watu binafsi na makampuni kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais. Mbali na leseni za uvuvi na uuzaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi, ushuru wa kuuza mazao ya uvuvi nje ya nchi, uliweka rekodi ambapo serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikusanya shilingi 18,544,735,905.20 sawa na asilimia 104.21 ya lengo kwa mwaka.

Aidha, ushuru wa kuingiza mazao ya uvuvi ndani ya nchi, nao ulipanda maradufu kwa kukusanywa shilingi 1,374,319,067.11 kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyowekwa na serikali hivyo kushawishi wananchi na taasisi mbalimbali kujiingiza katika sekta ya uvuvi ili kuongeza mapato kutokana na mahitaji makubwa ya mazao ya uvuvi nchini.

Vilevile, wizara imekuwa ikisimamia matukio ya uhalifu yanayohusiana na mazao ya uvuvi yakiwemo ya kudhibiti uvuvi haramu, matumizi ya zana haramu za uvuvi pamoja na utoroshwaji wa mazao ya uvuvi, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilikusanya shilingi 905,150,633.88 sawa na asilimia 95.99 ya lengo kwa mwaka kutokana na faini na makosa mbalimbali ya uvuvi huku ikiendelea kutoa elimu kwa wadau kutunza rasilimali za uvuvi zilizopo katika maeneo mbalimbali nchini.

Halikadhalika, wizara katika mwaka huo wa fedha ilikusanya shilingi 6,145,687,180.00 sawa na asilimia 92.02 ya lengo kwa mwaka kwa ajili ya vibali vya kusafirisha mazao ya uvuvi, hali inayoonesha kuwa mazao hayo yamekuwa yakihitajika kwa wingi ndani na nje ya nchi.

Bahari ya Hindi imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika pato la taifa kutokana na kuwa na aina mbalimbali za samaki, hali inayofanya meli kubwa kutoka nje ya nchi, kufanya shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 shilingi 3,266,252,013.46 sawa na asilimia 116.07 ya lengo kwa mwaka, zilikusanywa kutokana na leseni za uvuvi wa Bahari Kuu.

Maabara ya Taifa ya Uvuvi, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ilikusanya shilingi 1,259,047,006.25 sawa na asilimia 66.27 kupitia shughuli zake za utafiti wa sampuli za samaki na mazao yake yanayochakatwa ili kulinda afya ya mlaji.

Kambamiti ni moja ya mazao ya uvuvi yanayopatikana katika Bahari ya Hindi yenye thamani kubwa na kupendwa kuliwa ndani na nje ya nchi, ambapo kwa Tanzania walaji wengi ni wakazi wa Ukanda wa Pwani na katika mwaka wa fedha 2024/2025 leseni za uvuvi wa Kambamiti, ziliingizia serikali shilingi 57,667,146.15 sawa na asilimia 27.20 ya lengo kwa mwaka.

Mauzo ya vifaranga vya samaki aina ya sato, kutoka kwenye mashamba ya serikali ya Kilongwira (Morogoro), Mwamapuli (Tabora), Ruhila (Ruvuma) na Rubambagwe (Geita) yamewezesha kukusanywa shilingi 45,177,776.43 sawa na asilimia 13.69 ya lengo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Pia, serikali kupitia sekta ya uvuvi, imekuwa ikikusanya mapato mengineyo kupitia vyanzo mbalimbali, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilikusanya shilingi 137,859,611.53 sawa na asilimia 58.17 ya lengo kwa mwaka.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 bungeni jijini Dodoma Mei 23, 2025, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema wizara imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 74,105,001,000 katika mwaka huo.

Kati ya kiasi hicho, shilingi 38,105,000,000 zinatarajiwa kukusanywa kupitia sekta ya mifugo na shilingi 36,000,001,000 kupitia sekta ya uvuvi.

Mpango wa serikali ya awamu ya sita ni kuhakikisha sekta za uzalishaji zikiwemo za mifugo na uvuvi zinatoa mchango mkubwa zaidi katika ajira na pato la taifa, hivyo imekuwa ikiwezesha sekta za mifugo na uvuvi kuzalisha na kuuza kwa wingi ndani na nje ya nchi.



Dhima ya serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kushirikiana na sekta binafsi kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia ukuaji wa sekta za mifugo na uvuvi kuwa za kibiashara, kisasa na endelevu kupitia uandaaji na utekelezaji wa sera, mikakati, miongozo, usimamizi wa sheria, ufuatiliaji na tathmini, kujenga uwezo, weledi na ushirikishaji wa wadau wakiwemo wafugaji, wavuvi, wasindikaji, wachakataji na wafanyabiashara wa mifugo, uvuvi na mazao yake.

Malengo makuu ya wizara ni kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2025/2026, maduhuli yanaongezeka maradufu na kufikia malengo iliyowekewa ya kukusanya shilingi 74,105,001,000 kuanzia Julai 1, 2025 hadi Juni 30, 2026 hivyo inahakikisha inaendelea kusimamia programu mbalimbali zinazokuza ajira na kuhakikisha inakusanya mapato kupitia vyanzo vyake.

## SEKTA YA MIFUGO

**Kuanzia Julai 1, 2024 hadi Juni 30, 2025 sekta ya mifugo ilikusanya shilingi 35,658,450,089.79 sawa na asilimia 98.76 ya bajeti lengwa**

## SEKTA YA UVUVI

**Sekta ya uvuvi kuanzia Julai 1, 2024 hadi Juni 30, 2025, ilikusanya shilingi 32,669,985,272.28 sawa na asilimia 99 ya lengo**

# Wavuvi waanza kupewa elimu ulinzi rasilimali za uvuvi, Ziwa Victoria

**Na, Hamisi Hussein**



Timu ya watalamu wa Udhibiti Ubora na Masoko ya Mazao ya Uvuvi (QC) na Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (FRP) kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeanza utoaji wa elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi, uhifadhi ubora wa mazao ya uvuvi na umuhimu wa ulaji wa mazao ya uvuvi kwa wadau wa sekta ya uvuvi ukanda wa Ziwa Victoria ili kudhibiti uvuvi haramu na kulinda rasilimali zilizopo ndani ya ziwa hilo.

Timu hiyo ilianza utoaji elimu hiyo kwa wadau hususan wavuvi na wachakataji wa mazao ya uvuvi Agosti 23, 2025, katika mialo ya Wilaya za Nyamagana na Ilemela mkoani Mwanza mara baada ya kikao kazi cha kujadili mikakati ya pamoja ya kudhibiti uvuvi haramu ukanda wa Ziwa Victoria.

Akizungumza katika Mwalo wa Kayenze Kubwa uliopo Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza Afisa Uvuvi Mwandamizi Bw. Hamprey Tilla, aliwahimiza wavuvi kufuata sheria za uvuvi na kuuunga mkono jitihada za serikali kwa kuwa mabalozi na wadau muhimu katika kutafuta mikakati ya pamoja ya kudhibiti uvuvi haramu.





"Ndugu zangu sisi tunaongezeka lakini ziwa haliongezeki, tufuate sheria lakini sote kwa pamoja, nyie wavuvi, serikali na wadau wengine wote tunawajibu wa kulinda rasilimali hizi ndani ya ziwa letu." alisema Bw. Tilla.

Kwa upande wake Afisa Uvuvi Mkuu Bi. Gedrude Migodela, aliwahimiza wadau hao wa uvuvi umuhimu wa matumizi ya miundombinu bora ya kuhifadhia mazao ya uvuvi ili yaweze kukidhi vigenzo vya kimaabara kabla ya kuingizwa sokoni.

"Ni muhimu tukatumia njia bora kuhifadhi mazao yetu kwa sababu mazao haya yakipelekwa maabara yakibainika kuwa na changamoto zitokanazo na uhifadhi wake yatakosa soko." alisema Bi. Migodela.

Akiwa kwenye Mwalo wa Shadi Wilayani Nyamagana Afisa Mfawidhi wa Kituo cha Kudhibiti na Kusimamia Rasilinali za Uvuvi (FRP) Mwanza Bw. Hamad Stima aliwahimiza wadau wa uvuvi katika eneo hilo umuhimu wa utunzaji wa rasiliamli za uvuvi kwa ajili kulinda uchumi na afya za wananchi.

Pia, timu hiyo iliwakumbusha na kuwahimiza wadau hao juu ya umuhimu wa ulaji wa mazao ya uvuvi ambapo Afisa Uvuvi Mwandamizi Bi. Grace Kakama alisema familia nyingi za wavuvi zimekuwa hazitumii mazao ya uvuvi kama sehemu ya chakula chao kwa ajili protini.

Baadhi ya wavuvi waliuliza maswali mbalimbali wakati wakipokea elimu hiyo kutoka kwa wataalamu wa wizara na kuiomba serikali kufanya sensa ya wavuvi wote nchini kujua idadi yao ili waweze kupangiwa maeneo maalum ya kufanya shughuli za uvuvi, kupunguza idadi ya boti ikiwa ni sehemu ya maoni yao kuhusu utunzaji wa rasilimali za uvuvi kwenye ziwa hilo.

# Rais Samia adhamiria kutatua changamoto ya ajira kwa vijana



## Na. Edward Kondela

Serikali imekuwa ikiweka nguvu kubwa katika kuhakikisha inaongeza ajira kupitia sekta za uzalishaji pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kwa ajili ya uwekezaji na kutoa ajira hususan kwa vijana.

Kutokana na maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassa, katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita, alitoa maelekezo kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuanzisha Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ili kuwaandaa vijana na wanawake kuwa wawekezaji mahiri katika sekta ya mifugo na kuwawezesha kujiajiri.

Programu hii ilianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia Taasisi za Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) ikiwa imejikita katika kuongeza wigo wa fursa za ajira nchini kupitia sekta binafsi, uzalishaji na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya mazao yatokanayo na mifugo pamoja na kuongeza tija ya mifugo na pato la kaya na taifa kwa ujumla.

Wizara ilianza kutekeleza programu ya BBT kupitia vituo atamizi nane, vyenye jumla ya vijana 240 katika mikoa ya Tanga, Mabuki (Mwanza) na Kikulula (Kagera).

Aidha, wakati wa mafunzo, kila kijana alinenepesha ng'ombe mizunguko mitatu kwa mwaka kwa kunenepesha ng'ombe 10 kwa mzunguko mmoja pamoja na kupatiwa faida ya fedha itakayozalishwa katika kipindi cha uatamizi kupitia mizunguko hiyo.

Katika hali ya utekelezaji wa programu hiyo, jumla ya vijana 158 walifanikiwa kuhitimu mafunzo, huku serikali ikijenga na kukarabati miundombinu ya kuwezesha vijana makazi, mazizi, kuchimba kisima cha maji na miundombinu mingine muhimu.

Mambo muhimu ambayo vijana walifundishwa kuzingatia katika unenepeshaji ng'ombe ni pamoja na umri wa mnyama anayechaguliwa kunenepeshwa kuwa na miaka miwili hadi mitatu, bei ya ununuzi wa mnyama husika ambayo haitasababisha hasara, upatikanaji wa vyakula vya ziada, uwepo wa miundombinu muhimu ya unenepeshaji, matunzo kwa wanyama wanaonenepeshwa na soko la ng'ombe walionenepeshwa.

Halikadhalika, vijana walisaini mikataba na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na kupewa vitalu vya ekari 10 kila kijana ili kuanza uwekezaji, pamoja na kupatiwa mafunzo kuhusu namna bora ya kuandaa mipango biashara, uandaaji miundombinu ya unenepeshaji pamoja na uandaaji wa vyakula maalum vya unenepeshaji mifugo.

Pia, vijana walisaini mkataba mwingine na NARCO kuwa mnunuzi wa ng'ombe watakaonenepeshwa na vijana hao kwa shilingi 4,000 kwa kilogramu moja.

Vijana waliohitimu programu ya BBT, waliunganishwa na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi za fedha kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji mifugo kibiashara na serikali ilitenga na kutoa jumla ya shilingi 1,450,000,000 kwa ajili ya

# Rais Samia adhamiria kutatua changamoto ya ajira kwa vijana

kuwawezesha kuanza unenepeshaji mifugo katika Ranchi ya Kagoma, iliyopo mkoani Kagera.

Kupitia programu hiyo, jumla ya vikundi 20 vyenye vijana 106 walipatiwa ekari 1,761 katika Ranchi ya Kagoma na kupewa mkopo usio na riba wa jumla ya shilingi 934,231,000 kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa ajili ya kuendesha shughuli za unenepeshaji ng'ombe.

Vijana hao walianza kazi ya unenepeshaji wa ngo'mbe Mwezi Januari, 2025 ambapo hadi kufikia Mwezi Julai 2025, walinunua jumla ya ng'ombe 1,624 na kati ya ng'ombe hao walionenepeshwa waliuzwa jumla ya ng'ombe 1,078 ambapo katika kila ng'ombe aliyeuzwa hutengeneza faida ya kati ya shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000.

Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi 4,750,000,000 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu ya BBT hadi ngazi za mikoa mitano, ambapo wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kuwezesha vijana kujiajiri kwa kuwekeza katika shughuli za ufugaji, uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Kwa upande wa sekta ya mifugo, wizara imepanga kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana 240 kwenye vituo nane vilivyopo katika taasisi za LITA na TALIRI na kuanzisha vituo vipya viwili katika mikoa miwili.

Pia, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kutekeleza programu ya BBT kupitia mradi wa unenepeshaji wa mbuzi na kondoo, uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vitendo vya unenepeshaji wa mbuzi na kondoo kwa vijana na wanawake ili waweze kujiajiri katika mnyororo wa thamani.

Katika utekezaji wa programu hiyo, kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya machinjio ya kisasa ya mbuzi na kondoo, mabanda 10 yenye uwezo wa kufuga mbuzi 2,000 kwa wakati mmoja, mabucha 10, visima viwili vya maji, ofisi ya mradi, jengo kwa ajili ya majiko ya kuchoma nyama na vibanda vya kupumzikia wateja.

Vilevile, kutajengwa miundombinu ya ufugaji mbuzi na kondoo yenye uwezo wa kubeba mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja katika vitalu vya NARCO, pamoja na kujengwa miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji malisho na mbegu za malisho.

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, programu hiyo itaendelea kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kwa vijana 200 na kuwawezesha kupata mitaji.

Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora ni muhimu katika kuwezesha vijana kuwa wajasiriamali na wawekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi ambapo mafunzo yanayotolewa kupitia programu hiyo, yatasaidia kuzalisha vijana wenye ujuzi na weledi wa kuweza kuanzisha na kusimamia miradi binafsi sambamba na matumizi ya teknolojia stahiki zitakazowezesha kuongeza tija katika uzalishaji.





# Thamani ya mauzo sekta ya mifugo yapaa

**Na. Edward Kondela/Elibariki Mafole**

Katika miaka minne ya serikali ya awamu ya sita, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeendelea kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali nchini ambapo hatua hiyo ilichangia kuongezeka kwa thamani ya mifugo kutoka shilingi 30,489,866,668,000 kwa mwaka 2023/2024 hadi shilingi 33,216,845,677,000 Mwaka 2024/2025 kwa makundi yote ya mifugo.

Hali hiyo ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo katika kipindi cha marejeo mathalani idadi ya ng'ombe kwa asilimia 3.4 kutoka ng'ombe 37,913,129 hadi 39,241,375, mbuzi kwa asilimia 3.6 kutoka mbuzi 27,586,547 hadi 28,595,597 na kondoo kwa asilimia 3.2 kutoka kondoo 9,373,407 hadi 9,658,880.

Aidha, kuku waliongezeka kwa asilimia 5.0 kutoka 103,080,708 hadi 108,221,085, ambapo kuku wa asili waliongezeka kutoka 47,391,131 hadi 49,754,408 na kuku wa kisasa waliongezeka kutoka 55,689,577 hadi 58,466,677 na nguruwe waliongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka 3,901,096 hadi 4,131,962.



Pia, serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 9.4 kutoka tani 963,856.55 zenye thamani ya shilingi 9,476,474,305,000 mwaka 2023/2024 hadi tani 1,054,114.03 zenye thamani ya shilingi 10,378,706,595,000 mwaka 2024/2025.

Katika mwaka 2024/2025, kiasi cha nyama ya ng'ombe kilichozalishwa ni tani 666,227.02, nyama ya mbuzi tani 150,014.29, nyama ya kondoo tani 31,647.60, nyama ya kuku tani 147,449.98, na nyama ya nguruwe tani 58,775.14 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 612,808.50, mbuzi tani 134,403.35, kondoo tani 28,290.00, kuku tani 132,442.28, na nguruwe tani 55,912.42 kwa mwaka 2023/2024.

Ongezeko hilo lilichangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao, kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa, uboreshaji wa mbari za mifugo na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi.

Katika kutekeleza mkakati wa kukuza mauzo nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni, wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendelea kuratibu mauzo ya nyama kwenda nje ya nchi ambapo hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya tani 9,863.41 za nyama ziliuzwa sawa na asilimia 89.9 ya lengo la kuuza tani 10,971.

Kiasi hicho kinajumuisha tani 1,150.54 za nyama ya ngómbe, tani 6,380.63 za mbuzi, tani 2,104.85 za kondoo, tani 199.61 za nyama ya kuku na tani 27.83 za nguruwe zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 44.07 ziliuzwa katika masoko ya nje ya nchi ikilinganishwa na tani 9,326.3 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 39.3 zilizouzwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024.

Mauzo kwa mwaka 2024/2025 yaliongezeka kwa asilimia 5.75 ikilinganishwa na mauzo yaliyofanyika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita huku nyama ya mbuzi ikiendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 64.69 ya mauzo ya nyama nje.


Hali hii inatokana na jitihada zinazofanywa na serikali ya kuongeza ushirikiano na fursa za kibiashara nje ya nchi, masoko ya nyama yameendelea kuongezeka na kufikia nchi 11 ambazo ni Bahrain, Comoro, Hong Kong, Jordan, Kenya, Kuwait, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Vietnam.

Sekta ya mifugo imeendelea kuwa muhimu katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa taifa ambapo katika mwaka 2023, ilichangia asilimia 6.2 ya pato la Taifa (GDP) na kukua kwa asilimia 5.

Aidha, sekta hii inatoa ajira kwa kaya milioni 4.6 katika mnyororo wa thamani na kutoa mchango mkubwa katika uzalishaji wa malighafi za viwanda na kuchangia ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya mazao ya nyama na ngozi nje ya nchi.

Kuimarika kwa biashara ya mazao ya mifugo nchini kwa mwaka 2024/2025, kulichangia kuongezeka kwa ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka, mathalani kiwango cha ulaji wa nyama kutoka kilogramu 16 m waka 2023/2024 hadi kilogramu 17.6 Mwaka 2024/2025.



# MATUKIO KWENYE PICHA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena wakati wa utiaji saini mikataba na makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa vitotoleshi vya vifaranga vya samaki, ujenzi wa mifumo ya hewa kwenye mabwawa ya kufugia samaki, uchimbaji wa visima vya maji eneo la Kingolwira mkoani Morogoro na ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi Pangani mkoani Tanga hafla iliyofanyika ofisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mtumba, Dodoma Agosti 29, 2025.





Wataalam waliposhiriki shughuli mbalimbali za Wizara ikiwa ni pamoja na ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na serikali ili kuona maendeleo yake.










**MATANGAZO**



## BEI YA MBEGU ZA MALISHO
### (JUNCAO NA MAJANI TEMBO)

**Punguzo** Hadi **90%**

**SHILINGI ~~4,000~~ → Sh. 1000**

**Kwa mawasiliano zaidi:**

Vikuge (Pwani) - 0714060849
Langwira (Mbeya) - 0757637241
TALIRI - 0655420703
LITA - 0742762364

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Wizara ya Mifugo Na Uvuvi





## BEI YA VIFARANGA VYA SAMAKI
### (SATO)

**Punguzo** Hadi **50%**

Jinsi Moja (Monosex) Sh. ~~150~~ → Sh. 100
Jinsi Mchanganyiko (Mixed Sex) Sh. ~~100~~ → Sh. 50

**Kwa mawasiliano zaidi:**

Kingolwira (Morogoro) - 0787493792
Mwamapuli (Tabora) - 0779154377
Ruhila (Songea) - 0659669227

www.mifugouvuvi.go.tz



# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi